

Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa
Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

NGUVU ZA MFANO

“Basi kila asikiaye hayo maneno yangu, na kuyafanya, atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba” (Mathayo 7:24). Yesu Mwana wa Mungu alipotaka kupatia umati mfano wa kufananisha yale aliyokuwa akisema, aliwasimulia hadithi ya kuvutia, hadithi ambayo ilitumia lugha rahisi, lakini ambayo ilikuwa na uwezo wa kufanya watege sikio, na ikawa njia rahisi ya Yeye kuwawezesha kuelewa alichokuwa akisema. Basi bila hata kuwa na kisomo na shahada ya thiolojia, na bila kusomea mafunzo kuhusu kanuni bora za kutoa hotuba mbele ya watu, Yeye Mpakwa Mafuta wa Mungu alifundisha vikundi tofauti vya umati wa watu kwa kutumia hadithi zilizohusiana na maisha ya kila siku, ambazo zilifunulia wasikilizaji wake kweli kubwa za kiroho. Hadithi hizo zilisimua mawazo yao na kuhuisha roho zao, hisia zao, na fikra zao. Na wakati alipomaliza kuwatolea mfano ule wa mtu mwenye akili na mtu mpumbavu, “Makutano walishangaa mno kwa mafundisho yake; kwa maana alikuwa akiwafundisha kama mtu mwenye amri, wala si kama waandishi wao” (28-29).

Nyingi za hadithi ambazo Yesu alihadithia, na ambazo kamwe hazingeweza kusahaulika, hujulikana kama mifano. Maana ya neno mfano ni kifananishi, au maelezo ya jambo kwa njia ya hadithi inayotumia maisha ya kawaida, na ambayo hutumika kufundisha somo fulani, tabia fulani, au wajibu fulani ambao mtu anahitaji kutimiza. Neno la Kiyunani ambalo linatumiwa kumaanisha mfano “linaashiria kitu ambacho kimewekwa kushahabiana na kingine . . . maanake kuweka kitu kimoja kando ya kingine kwa lengo la kulinganisha” (Kamusi ya Vine, ya Kuelezea Maana ya Ndani). Na kama vile kamusi ya Thayer inavyosema, “Mfano ni hadithi ya kilimwengu ambayo ina maana kwa mambo ya mbinguni.” Mfano ni malinganisho au sampuli inayotumia mambo ya kawaida ya dunia au ya hali za kibinadamu kufundisha somo la kiroho. Katika mafundisho yake Yesu alitumia vifananishi na hadithi za maisha ya kawaida ambayo yalitokana na utamaduni alikoishi. Basi akafundisha ukweli kuhusu mambo ambayo watu hawakujua kwa kuyalinganisha na mambo ya kawaida ambayo watu walijua. Akatoa

maelezo na kufafanua ukweli mkuu kwa kutumia mambo ambayo watu waliona kila siku maishani mwao, kama vile masomo kuhusiana na mkulima aliyepanda mbegu, au msafiri mwenye kupita njiani kuelekea Yeriko (Msamaria Mwema). Mafafanuzi hayo yalitumia maisha ya kawaida ndiposa yakawa yanafaa sana kuwasaidia wasikilizaji wake kuelewa maana ya ukweli ule ambao walikuwa wakifundishwa.

Zaidi ya thuluthi moja ya mafundisho ya Yesu yalifundishwa kwa kutumia mifano. Nyingi za hadithi hizo zilikuwa ni rahisi kueleweka. Hata ingawa mara nyingi mifano ya Yesu ilitumia maneno mengi, kila mfano ulitolewa kufundisha ukweli mmoja tu au ujumbe mmoja tu. Yesu Kristo ambaye ni Mwalimu wetu Mkuu ni mfano bora wa kufuata hata katika hizi siku zetu. Mafundisho yake yaliyotokana na Roho Mtakatifu, na ambayo yalitumia mafafanuzi mengi, yalikuwa chimbuko la masomo mazuri ya kiroho ambayo si rahisi kusahau.



Ni rahisi kuelewa na kukumbuka mifano ya Yesu hata zaidi ya kukumbuka mafundisho mengine ya kithiolojia. Mifano hiyo husema mengi kuhusu Mungu, sifa zake, ufalme wa Mungu, n.k. Kweli nyingi kuhusu Itikadi za Ukweli hupatikana kutokana na mifano hii rahisi. Hadaa zinazoletwa na dhambi, na msamaha ambao Baba hupatia watu wake, ni mambo ambayo huwezi kusahau baada ya kusoma mfano wa Mwana Mpotevu. Nao umuhimu wa maombi unawekewa wazi akilini mwetu kwa kusoma mfano wa mjane ambaye hakuona aibu kwenda mara baada ya nyingine mbele za hakimu mkatili, huku akitafuta haki yake. Na hadithi ya wanawali kumi daima hutukumbusha umuhimu wa sisi kuwa tayari kwa sababu ya kurudi kwake mwenye husi, wakati ambao hatutakuwa tukitarajia. Hadithi ya kondoo aliyepotea inadhihirisha sifa za upendo wake Mwokozi ambaye kamwe hakomi kutafuta waliopotea. Kwa kweli mifano hii ya Kristo inapendeza sana na ni vito vya ukweli ambavyo Wakristo wanastahili kujifunza kutokana navyo, na pia kufundisha watu wengine kupitia kwake. ■

Lengo La Mifano

Tahariri

Mifano Ya Yesu

Mwongozo wa
Kujifunza Mifano
6-7

Je, Wajua?

Mafafanuzi Ambayo
Hutumiwa Katika
Mahubiri

Mchoro Wa Kristo

Neno Linalofaa kwa
Msimu Huu

MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

Neno la Mungu

2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

Uhusiano wa Upendo

Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

Toba

Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

Uzao Mpya

Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4,
Efe. 2:1, 5-6

Uhuru Kutokana na Dhambi

1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

Ujazo wa Roho Mtakatifu

Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

Utakatifu

Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16,
Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

Ufalme wa Mungu

Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

Kanisa

Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13,
Kol. 1:18

Umoja

Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

Kanuni za Kanisa

Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27,
Yn. 13:14-17

Uponyaji wa Kiungu

Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

Utakatifu wa Ndoa

Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3,
I Kor. 7:10-11

Urembo wa Nje

I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

Mwisho wa Nyakati

2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10,
Mt. 25:31-46

Kupenda Amani

Lk. 6:27-29, 18:20

Ibada

Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

Wajibu Mkuu

Mk. 16:15

LENGO LA MIFANO

Yesu alitumia mifano aidha kufundisha ukweli au kujibu swali. Yeye alitumia hali za kawaida za wanadamu ili kusaidia wasikilizaji wake kuelewa aliyokuwa akifundisha. Wakati mmoja mwana-sheria alisimama mbele yake na kumuuliza: “Jirani yangu ni nani” (Luka 10:29). Hapo hapo Yesu akaanza kumhadithia hadithi ya Msamaria Mwema. Ndiposa baadaye akamuuliza, “Waonaje wewe, katika hao watatu, ni yupi aliyekuwa jirani yake yule aliyeangukia kati ya wanyang’anyi” (aya ya 36). Jibu la swali hilo lilikuwa dhahiri kutokana na hadithi ambayo Yesu alikuwa amehadithia, lakini hadithi yenyewe ilifanya wasikilizaji wake kuwaza na kuwazua

jambo hilo kibinafsi. Jambo hili basi likazua ukweli kutoka kwa watu ambao pengine wangeukataa ukweli huo kama ungelisemwa kwa njia ya moja kwa moja.

ILIZUA ILIDHIHIRISHA ILIFICHA ILIHIFADHI

Wakati mwingi mifano hiyo ya Kristo ilidhihirisha ukweli kwa njia ambayo usemi wa moja kwa moja haungefaulu kufanya. Watu walio na roho za kweli na ambazo zinatafuta ukweli watasikia na

kuelewa mambo haya. Kutoa mifano ni njia ambayo inafaa ya kuwasilisha na kudhihirisha ukweli kwa njia rahisi ya kuelewaka; kama jinsi ambavyo mfano wa Msamaria Mwema uliohadithiwa hapo juu unavyofaulu kufanya.

Mifano mingine ambayo Yesu alihadithia ilisemwa kwa njia ambayo ilificha ukweli kwa watu wale ambao walikuwa wamechagua kuendelea kuishi gizani. “Wakaja wanafunzi, wakamwambia, Kwa nini wasema nao kwa mifano? Akajibu, akawaambia, Ninyi mmejaliwa kuzijua siri za ufalme wa mbinguni, bali wao hawakujaliwa. Kwa maana ye yote mwenye kitu atapewa, naye atazidishiwa tele; lakini ye yote asiye na kitu, hata kile alichochacho atanyang’anywa. Kwa sababu hii nasema nao kwa mifano; kwa kuwa wakitazama hawaoni, na wakisikia hawasikii, wala kuelewa” (Mathayo 13:10-13). Huenda ikawa muumini ameshindwa kuelewa lengo kuu la mfano kwa sababu ukweli wake ulikuwa umefichwa kutoka kwa wale ambao “hawakuwa na masikio ya kusikia.” Basi lilikuwa jambo la kawaida kwa wanafunzi kurudi kwake Kristo na kuomba kupewa maelezo zaidi ya kindani kuhusu mfano aliotumia.

Ni jambo rahisi mtu kuweza kukumbuka mifano kwa sababu ilitumia maneno ambayo yalichora picha timamu ya jambo lililokuwa likizungumziwa. Hii ndio sababu mifano huwa muhimu katika kutuwezesha kukumbuka kweli za kiroho. Kwa kweli mifano ya Yesu ilikuwa (na ingali) vito na hazina muhimu vya kuhifadhi ukweli kwa manufaa ya watu na tamaduni tofauti tofauti. ■

Gazeti la *Ukweli wa Injili* ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwahimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tutembelee katika tovuti yetu ya www.thegospeltruth.org na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uweze kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika nchi nyingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kupitia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako.

—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@the-gospeltruth.org

Tahariri



Kwa mifano mingi ya namna hii alikuwa akisema nao neno lake, kwa kadiri walivyoweza kulisikia; wala pasipo mfano hakusema nao; lakini akawaeleza wanafunzi wake mwenyewe mambo yote kwa faragha. — Mariko 4:33-34

Katika robo hii ya mwaka yake toleo hili la Ukweli wa Injili linaangazia mifano yake Yesu. Mifano ilikuwa sehemu muhimu ya mafundisho yake Kristo, na ni kipengele muhimu cha kutumia kufundisha Ukristo hata katika siku zetu. Mifano hufafanua ukweli kwa njia ambayo usemi wa moja kwa moja hakuwezi kufikia. Hata ingawa Yesu hakupaka mafuta mafundisho yako, Yeye aliguzia undani wa maswala ambayo yalikuwa watu wa wakati huo kwa njia rahisi. Wakati mwingi wasomi wa Biblia na wanathiolojia huwa na ubishi mkubwa wa kukubaliana maana ya mifano ya Yesu, na pia kutokubaliana ni kitu gani hufanya hadithi moja kuwa mfano ilhali ingine ikiwa ni hadithi ya kawaida tu (ya kufafanua jambo). Lakini mfano ulio wa kweli ni hadithi ambayo ina ukweli ndani yake ambao umefichika, na pia ndani mwake kuna malinganisho ya matukio ya kawaida na somo la kiroho.



Tutembelee

www.thegospeltruth.org

ili kujiandikisha na

kupata jarida

za mbele.

Mzigo ambao niko nao ni kuhimiza watu kujifunza mifano ya Yesu, na wajitumbukize ndani ya mafundisho yanayopatikana kutokana na mafafanuzi ambayo Kristo alisimulia. Ukweli ni kwamba, kila mmoja wetu hutumia njia tofauti kujifunza, lakini Kristo alionelea ni jambo muhimu Yeye kuweza kuwafikia watu wa kizazi chake kwa kutumia hadithi za mifano ili wao waweze kuelewa ukweli aliokuwa akiwapa.

Miaka kadhaa iliyopita nilipata mweke spesheli wa kufanya mkutano wa siku kadhaa na kikundi kimoja cha wachungaji katika Afrika. Katika vikao vya hapo mbeleni tayari tulishakuwa na wakati na vipindi vya kufundisha na kujifunza kwa pamoja itikadi za Ukristo. Lakini sasa nilijihisi kwamba tulihitaji kufanya jambo tofauti. Mungu alikuwa amenipatia ufunuo mpya kuhusiana na nguvu za mifano. Macho yangu yakafunguka na kuona kweli za ajabu ambazo hupatikana katika mifano yake Kristo. Kwa siku nyingi wahudumu hawa walijifunza mifano hiyo na kushiriki kwa pamoja kweli ambazo walikuwa wakijifunza katika kikao hicho. Mimi nami nikajisikia kubarikiwa sana kwa kupata nafasi ya kushiriki na wao kweli kuu ambazo zilitokana na ripoti ambazo zilitolewa na kila kikundi kwenye kikao hicho, kweli ambazo zilihusu nyanja tofauti tofauti za Ukristo (kama vile): maombi, msamaha, wokovu, upendo wa Mungu, hukumu, dhambi, ufalme wa Mungu, rehema, uzima wa milele, mbingu, jehanamu, uinjilisti, na mengine mengi. Kuna mafundisho mengi ya kiitikadi na ukweli ambayo yanapatikana kutokana na hadithi hizi; na hadithi zenyewe zinafaa kwa kuwapatia watu ukweli kwa njia ambayo vikao vya mihadhara ya 'moja kwa moja' haviwezi kufikia.

Ni ombi langu kwamba Mungu atakuvuvia ili uweze kujifunza mifano ya Yesu na kuweza kujua utajiri na uwezo ambao hupatikana ndani mwake.

Michael W. Smith

Aprili 2021.

MAFAPANUZI AMBAYO HUTUMIWA KATIKA MAHUBIRI



Mafafanuzi ya kisasa na hadithi za maisha ya kawaida ni vipengele muhimu katika kufanya wasikilizaji wako kuelewa mahubiri yako. Mafafanuzi hayo yanaweza kufanya washirika wako kukuelewa na pia kufanya ukweli kuaminika katika hali na tamaduni za kisasa. Lakini hata ingawa kutoa hadithi kunaweza kuwa silaha muhimu ya kuwawezesha watu kuelewea kile ambacho unahubiri, mhadumu wa Kristo kamwe hastahili kuwa mchekeshaji wa watu, au mtu mwenye sarakasi za kuwafurahisha watu. Kazi yetu ni kuhubiri Neno lake Mungu. Kama hadithi fulani itasaidia katika mahubiri hayo

basi isimulie, lakini usiruhusu hadithi kuwa muhimu hata zaidi kuliko ukweli wenyewe.

Pia ni jambo muhimu kwamba, wakati unapotoa mafafanuzi yako, kamwe usijaribu kufanya kitu kuwa cha kweli eti kwa sababu "kinalingana" na mfano wako au hadithi yako. Wahubiri wengi hufanya makosa ya kubadilisha umuhimu wa ukweli kwa kufanya mafafanuzi wanayotumia kuwa na umuhimu zaidi. Lakini jambo fulani huwa ni la kweli kutokana na yale ambayo Neno la Mungu linasema, si kwa sababu sisi wenyewe tumetoa hadithia fulani ya kupendeza ambayo tunajaribu kuunda ukweli kutoka ndani yake. ■

MIFANO YA YESU

“Akawatolea mfano mwingine, akisema. . .”

Mfano	Mathayo	Marko	Luka
Ufalme wa Mbinguni			
Mpanzi	13:3-8, 18-23	4:4-8, 14-21	8:5-8, 11-15
Mbegu ya Haradali	13:31-32	4:30-32	13:18-19
Chachu	13:33		13:20-21
Hazina Iliyofichika	13:44		
Lulu Nzuri	13:45-46		
Mbegu Inayomea na Kukua		4:26-29	
Hali ya Kuwa Mtu Mpotevu na ya Kupata Ukombozi			
Kondoo Aliiyepotea	18:10-14		15:1-7
Sarafu Iliyopotea			15:8-10
Mwana Mpotevu.			15:11-32
Kutii/Kutotii			
Nyumba Iliyojengwa Juu ya Mwamba	7:24-27		6:47-49
Wana Wawili	21:28-32		
Watumwa Wasio na Faida Yoyote			17:7-10
Usimamizi			
Talanta	25:14-30		
Msimamizi Asiyeye Mwaminifu			16:1-13
Mafungu Kumi ya Fedha			19:11-27
Kristo			
Wakulima Waovu	21:33-45	12:1-12	20:9-19

Kondoo Aliiyepotea



Mpanzi na Mbegu



Mfano	Mathayo	Marko	Luka
Kuomba			
Rafiki Anayefika Usiku wa Manane			11:5-13
Hakimu Ambaye Si Mwenye Haki			18:1-8
Mfarisayo na Mtoza Ushuru			18:9-14
Upendo na Huduma kwa Wengine			
Msamaria Mwema			10:30-37
Kusameheana			
Mtumishi Asiyesamehe	18:21-35		
Wadeni Wawili			7:41-43
Matukio ya Siku za Mwisho/(Mtu) Kuwa Tayari			
Magugu	13:24-30, 36-43		
Wavu wa Kuvua Samaki	13:47-50		
Wafanya kazi katika Shamba la Mizabibu	20:1-16		
Karamu ya Arusi	22:1-14		
Tajiri Mpumbavu			12:16-21
Watumwa Waangalifu		13:34-37	12:35-40
Mtumwa Mwaminifu/ Asiye Mwaminifu	24:45-51		12:42-48
Wanawali Kumi	25:1-13		
Mtini Usiozaa Matunda			13:6-9
Karamu Kubwa			14:15-24

HADITHI NA MAFAFANUZI KADHA WA KADHA



Sarafu Iliyopotea

Hadithi/Mafafanuzi	Mathayo	Marko	Luka
Chumvi ya Dunia	5:13	9:50	14:34-35
Taa (Juu ya Kiango)	5:14-16	4:21-22	8:16-18
Jicho na Mkono wa Kumfanya Mtu Kufanya Makosa	5:29-30; 18:8-9	9:43-47	
Kuweka Hazina	6:19-21		
Ndege wa Angani na Maua	6:25-34		12:22-32
Mchungaji Mwema	Yohana 10:1-16		
Kibanzi na Boriti	7:1-5		6:41-42
Mlango Mwembamba na Mpana	7:13-14		
Ngamia/Tundu la Sindano	19:23-24	10:23-25	18:24-25
Kikombe na Chano	23:25-26		11:37-39
Kondoo na Mbuzi	25:31-46		
Kiti cha Nyuma			14:7-14
Kujenga Mnara/Kwenda Vitani			14:25-33
Tajiri na Lazaro			16:19-31

MWONGOZO WA KUJIFUNZA MIFANO

Kujifunza kutokana na mifano ni njia bora ya kuvutia na ambayo ina uwezo mkubwa wa kumwezesha mtu kuelewa itikadi nyingi za Ukristo, na pia mafundisho yake Kristo. Mifano sio hadithi tu; ni njia bora ya kufundisha inayolingana na maisha ya kila siku, na ambayo inaangazia kweli kuu za mafundisho ya Ukristo. Lakini kusudi kuu la ukweli ambao mtu hujifunza kutokana na mfano hauwezi kamwe kwenda kinyume na mafundisho makuu yanayopatikana katika Biblia; ukweli ni kwamba, maaandiko na unabii ambao wakati mwingine ni mgumu kueleka katika Biblia unahitaji kutafsiriwa kwa njia ambayo inakubaliana na mafundisho ya Kristo, ambayo yalikuwa rahisi kueleweka. Ni muhimu sisi kuchunguza mifano kwa njia ya kweli na uwazi ili kuweza kuelewa umuhimu wake kwa njia ya undani zaidi. Vidokezo ambavyo vimetolewa hapa chini vinaweza kumpatia mtu mwongozo bora wa kuweza kuelewa mifano ya ajabu ambayo Yesu alisimulia.



Talanta

“Maana ambayo mifano unapewa inahitaji kulingana na Maandiko yale mengine na pia ilingane na mafundisho ya Kristo na ya mitume.”

Weka Maanani Muktaadha wa Maandishi

Zingatia muktaadha wa mfano unaochunguzwa. Chunguza kile ambacho kimesemwa kabla ya mfano huo kuhadithiwa na baada yake kuhadithiwa. Wakati mwingi Yesu alieleza bayana kusudi na maana ya mfano aliosimulia. Kwa mfano -- mfano wa mjane ambaye hakukoma kuitisha haki yake kutoka kwa hakimu unaweza kueleweka vibaya ikiwa mtu hatachunguza muktaadha wake. Mtu anaweza kuchukulia kwamba hadithi hiyo inamwonyesha Mungu ambaye si wa haki, na ambaye hajali watu. Lakini hayo sio mambo ambayo yanafundishwa katika mfano huo; Yesu mwenyewe aliweza kutoa kusudi la mfano huo katika mstari wa kwanza wa aya hiyo: “Akawaambia mfano, ya kwamba imewapasa kumwomba Mungu sikuzote, wala wasikate tamaa.”

Chunguza Mambo Yote Yalioandikwa kwa Njia Ambayo Inafaa

Mifano kadhaa huwa na maelezo ambayo hayana umuhimu mkubwa wa kiroho. Maelezo hayo yameandikwa humo ili kufanya hadithi ileleweke na kumchorea msomaji picha ambayo inafanua kweli kuu ambayo inafundishwa. Mfano wa hakimu ambaye hakuwa mwenye haki haisemi kuhusu Mungu, bali maelezo yaliyomo ndani yake yametolewa ili kuonyesha ukakamavu na mwelekeo wa kutokufa moyo wa mjane huyo, ambaye ndiye mhusika mkuu kwenye mfano. Basi wewe kuwa makini ili usipatie umuhimu wa kiroho kila jambo ambalo limeandikwa kwenye mfano ambao unajaribu kuelewa.

Imesemekana kwamba sio kila kitu katika mfano kina maana fulani. Kila jambo lililosemwa humo sio somo maalum, na sio sampuli ya mambo yanayofundishwa

ndani mwake. Hii ni kumaanisha kwamba sio wakati wote ambapo mifano huwa fumbo la kufumbuliwa, kwa sababu si yote yaliyosemwa humo ndani huwa na maana ya kiroho. Kujaribu kupatia maana mambo yote yaliyosemwa ndani ya mfano ni jambo ambalo laweza kumpotosha mtu na kumfanya asipatie maana kamili ya mfano.

Kuwa Makini kwa Michoro au Picha Zinazorudiwa-rudiwa

Wakati mwingi michoro ambayo Yesu alitumia imerudiwa-rudiwa katika Maandiko, na huwa na maana inayofanana kutoka mfano mmoja hadi mwingine. Mara nyingi mchoro wa ‘Bwana, Hakimu, au Mfalme’ ulitumiwa kumwakilisha Mungu. Nao mchoro wa wafanyi kazi na watumishi ulitumiwa kuwakilisha wafuasi wa Mungu. Kondoo nazo angalau ziliwakilisha watoto wa Mungu, ilhali mbuzi huwakilisha wale ambao hawajakombolewa. Aidha mchungaji, mwangalizi wa shamba la mizabibu, au mwana wa mfalme – ni mchoro ambao wakati mwingi hutumiwa humwakilisha Kristo.

Ni Kwa Nini Mfano Ulitolewa?

Wakati mwingi Yesu alitoa mfano ili kujibu swali aliloulizwa au kukabiliana na mwelekeo fulani ambao waliomzunguka walikuwa nao. Katika Luka 15 Yesu alisimulia kuhusu mifano ya kondoo aliyepotea, sarafu iliyopotea, na mwana mpotevu. Yesu alitoa mifano hiyo ili kuwajibu Mafarisayo na Waandishi wa Sheria ambao walikuwa wakinung’unika huku wakisema “Mtu huyu huwakaribisha wenye dhambi, tena hula nao” (aya ya 2). Kuelewa chimbuko la mifano ni jambo ambalo litamsaidia mtu kuelewa wazo linalozungumziwa katika mfano wenyewe. Basi lengo la mifano hii lilikuwa kuonyesha vikundi hivyo mwelekeo wa Mungu kwa wenye dhambi.

Tafuta Wazo Moja Kuu

Mifano ilitolewa ili kutilia nguvu wazo fulani. Unaposoma mifano ya Yesu chunguza kwa makini ukweli mkuu ambao alikuwa akiwasililisha, lakini pia usisahau muktadha au sababu ya Yeye kutoa mfano huo. Na ili uweze kukaza akili zako katika wazo kuu linalofundishwa hebu tafakari na ujibu maswali yafuatayo:

1. Je, malinganisho makuu yanayopatikana katika mfano huo ni yapi?
2. Wahusika wakuu ni akina nani?
3. Ni nani au ni kitu gani kinaangaziwa sana katika mfano wenyewe?
4. Ni jambo gani linalotokea baada ya mfano kutolewa?

Chunguza Mandhari ya Utamaduni na Historia ya Wakati Huo

Mtu anaweza kuelewa mfano kwa njia bora zaidi ikiwa ana ufahamu wa mandhari ya kihistoria na utamaduni wa wakati huo. Baadhi ya mifano hulingana na tukio au mazoea ambayo yalieleweka na Wayahudi wa wakati huo. Hapa tunaweza kutoa mfano wa karamu ya harusi ambayo inapatikana katika Mathayo 22:1-14. Yule bwana ambaye hakuwa na vazi la harusi alitupwa nje ambako mlijaa giza totoro. Baadhi yetu tunaweza kujihisi vibaya kuona yaliyofanyiwa maskini huyo ambaye pengine hakuwa na uwezo wa kupata nguo inayofaa, hadi wakati ambapo tunaelewa kwamba wakati ambapo Yesu alihadithia mfano huo utamaduni ulimbidi Bwana harusi kuwapatia wageni wake mavazi ya harusi. Ukweli ni kwamba, mtu huyo alikuwa ameamua kutovaa mavazi ambayo alikuwa amepewa. Basi hapo ndipo tunaelewa zaidi mafundisho ya ukweli kuhusu jehnamu na adhabu ambayo hupatikana kwenye mfano huu.

Maana ya Mfano

Maana ambayo mfano unapewa inahitaji kulingana na Maandiko yale mengine na pia ilingane na

mafundisho ya Kristo na ya mitume. Hata ingawa ukweli unaweza kuimbuka kutokana na hadithi au mfano, msomaji anahitaji kuwa mwangalifu ili asijenge itikadi zake kutokana na maana ambayo haifai ambayo pengine mfano huo umepewa. Kwa kweli mfano huwa ni malinganisho kati ya mambo mawili. Kama mfano unahusiana na ufalme wa Mungu, basi maana inayotolewa inastahili kulingana na ufalme wa Mungu, sio kuambiwa jinsi mfano huo unahusiana na familia, matukio ya kisiasa, n.k. Zingatia kabisa kwamba nyingi za mifano huwa na maana moja peke yake.

Katika historia watu wamepatia mifano (mingine) maana ya kimchezo na ya kimafumbo. Hili ni jambo ambalo ni kinyume na lengo la kutolewa kwa mfano huo au lengo linaloashiriwa na mfano wenyewe.

Ndiposa Martin Luther akaandika na kusema kwamba, maana zingine ambazo zimetolewa kwa mifano ni “upuzi mtupu” ambao “kamwe haufai!”



Wanawali Kumi

Baada ya Kuchunguza Mfano Utumie Maishani Mwako

Baada ya kusoma mfano na kuchunguza maana yake halisi, ni muhimu kutumia mafundisho yake maishani mwako. Je, mfano huo unanifunza nini kuhusu ufalme wa Mungu na mambo ambayo yatakuja baadaye? Je, ukweli huu unahusiana kwa njia gani na maisha yangu? Mungu angetaka nifanye nini?

Kujifunza mifano ni jambo ambalo litaleta baraka kubwa, changamoto, na hata himizo kwa wasomaji wake. Hebu basi tutafute ili tuweze kujua, tujifunze ili tuweze kuelewa, na tufanye juu chini kuweza kumjua Mungu ili Bwana wetu atakaporudi atupate tukiwa waaminifu. ■

Mchoro wa Kristo

Injili ya Yohana inafanya bidii kutuchorea mchoro wa Yesu ambayo ni dhahiri, sifa zake, na hata maumbile yake. Kuna semi (tamathali za usemi au vifananishi) tisa ambazo Yohana alitumia kumweleza Yesu.



1. MIMI ni Mkate wa Uzima/Uhai — Yohana 6:35, 48, 51.
2. MIMI ni Nuru ya Ulimwengu — Yohana 8:12; 9:5.
3. Ibrahimu Asijakuwako, MIMI Niko — Yohana 8:58.
4. MIMI Ndimi Mlango — Yohana 10:7, 9.
5. MIMI Ndimi Mchungaji Mwema — Yohana 10:11, 14.
6. MIMI Ndimi Ufufuo na Uzima — Yohana 11:25.
7. MIMI Ndimi Njia, Ukweli, na Uzima — Yohana 14:6.
8. MIMI Ndimi Mzabibu wa Kweli — Yohana 15:1, 5.
9. Ni MIMI. — Yohana 18:5-6.



JE, WAJUA?

Mingi ya mifano ya Yesu inapatikana katika injili zile ambazo zinafanana (Mathayo, Marko, na Luka). Hata ingawa Injili ya Yohana ina hadithi na mafafanuzi kadha wa kadha, humo ndani mwake hamna mifano ya kweli. Yohana 10:6 inatumia neno “mithali,” neno ambalo kwa lugha ya Kiyunani lina tofauti ya maana na lile ambalo limetumiwa kumaanisha neno “mifano” ambalo maana yake ni jambo au usemi wa kufananisha.



LULU YA THAMANI KUBWA

Tena ufalme wa mbinguni umefanana na mfanya biashara, mwenye kutafuta lulu nzuri; naye alipoona lulu moja ya thamani kubwa, alikwenda akaauza alivyo navyo vyote, akainunua. — Mathayo 13:45-46

Lengo la mfanya biashara ni kununua na kuuza bidhaa ili aweze kupata faidha ya juu zaidi ambayo anaweza kupata. Kwa karne nyingi watu wamevuka bahari kubwa na kuweza kuchunguza nchi mpya katika jitihada za kutafuta hazina na utajiri huku wakihatarisha maisha yao. Shida na hatari ambazo walizikumba zilionekana gharama ndogo kulipa ikilinganishwa na uwezekano wa wao kupata utajiri mkubwa wa kidunia.



Yesu alitoa mfano huo kufafanua kuhusu wokovu ambao humtoa mtu dhambini na kumpatia zawadi ya uzima wa milele ambayo ni kama lulu ya thamani kuu. Wakati mfanyi biashara anapopata lulu ya hali hii yeye huuza mali yake yote ili aweze kununua kile ambacho ni cha thamani kuu zaidi. Wokovu ni kitu cha thamani kubwa kuliko lulu yoyote ile ya kawaida. Anayetafuta wokovu anahitaji kuacha mambo mengine yote ya kidunia kwa ajili ya furaha na tabasamu anazopata moyoni mwake, huku akiendelea kumtafuta Kristo na ukombozi wake kutoka dhambini. Lulu hii ya ajabu hupatikana tu wakati ambapo tunaitafuta kwa mioyo yetu yote.

Wakristo ambao ni wavivu na ambao hawana mpango kabambe wa uhusiano wao na Mungu – aidha iwe kwamba hawajapata wokovu huo wa kweli, au wako katika hatari ya kupoteza kile ambacho tayari washapata. Lakini ili mtu aweze kumfuata Yesu anahitaji kuachana na mambo yale mengine yote, ili aweze kupata nguvu na furaha ya wokovu wa kweli. Kwa kweli tunastahili kutafuta lulu hiyo ya thamani kubwa kwa mioyo yetu yote bila kujibakishia chochote kile.

Tunapopata lulu hiyo ya thamani kubwa ambayo ni wokovu wetu kutoka dhambini, na pia kupata tumaini la uzima wa milele, lulu hiyo huandamana na amani ya ndani, na pia furaha ambayo mtu hawezi kupata kutoka kitu kingine chote ulimwenguni. Sisi kama watumishi wa Bwana tunahitaji kuwasilisha ujumbe wa thamani ya kweli na umuhimu wa wokovu. Ni ombi letu kwamba maisha yetu yatadhihirisha utajiri na furaha ya wokovu kamili. Adui yetu anataka tuweke mawazo yetu kwenye fikra kwamba inatubidi kuuza mali yetu yote, badala ya kuwazia hazina ya thamani kubwa ambayo hupatikana ndani mwake Yesu Kristo.

Kama wewe umeokoka na unamjua Yesu Kristo basi una lulu ya thamani kuu. Hebu basi enda ukamweleze mtu mwingine kuhusu wokovu huu mkuu ili naye aweze kupata uzima huo wa milele. ■

Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

UTAKATIFU KWA BWANA